

Pambazuko

Toleo Namba 051

Jumatatu Oktoba 23-29, 2023



**Makonda wa JPM vs
Makonda wa Samia**

Uk. 5



**Rostam
apeleka
umeme
Zambia**

Uk. 6



**Changia
uhai wa
Pambazuko**

Uk. 4

Deni la taifa 'layeyuka'

Uk. 14

JISAJILI HAPA: Andika neno **HABARI** na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Rais Samia achukue hatua kali

JUMATANO ya Machi 29, mwaka Jhuu Rais Samia Suluhu Hassan alionyesha hasira zake kwa umma kwa kutamka maneno makali.

Akipokea ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali (CAG), jijini Dar es Salaam, Rais Samia alikerwa mno na kuwepo kwa kila dalili za rushwa, wizi na ubadhirifu ambazo zimesheheni ndani ya taarifa hiyo aliyokabidhiwa.

Katika uongozi wake wa miaka mwili, kwa mara ya kwanza, Watanzania na dunia walishuhudia namna ambavyo Rais Samia hapendi rushwa, wizi na ubadhirifu. Alifika huku sura yake ikionekana “kuvaa” hasira.

Rais Samia alifika wakati akatumia maneno makali ya Kiingereza; “stupid” – akimaanisha upumbavu mkubwa kwa baadhi ya watendaji wa serikali ambao wamekuwa wakishindwa kutumia uzalendo katika kuwajibika, badala yake wamekuwa wakiamini dhamana zao ni chumo lao kwa manufaa binafsi.

Pamoja na Pambazuko kupongeza hasira hizo za Rais Samia, bado tunaamini kwamba hasira pekee hazitoshi kuwakemea Watanzania wengi kuacha rushwa, kujihusisha na ubadhirifu na hata matumizi mabaya ya dhamana walizokabidhiwa kwa niaba ya wananchi.

Rais Samia amekuwa sehemu ya utendaji wa serikali kwa muda mrefu, hivyo tunaamini anatambua wapi kuna mianya mingi ya rushwa ubadhirifu na uchafu mwingine ambao unachafua taswira ya serikali yake kwa umma wa Waanzania na dunia.

Kimsingi, wanaotenda maovu hayo, wanamchongea Rais Samia kwa wananchi, na kumuonyesha kwamba ni kiongozi asiye chukua hatua kunapotokea uchafu katika utendaji wa serikali.

Kama ambavyo wananchi wengi wanapendekeza Rais Samia kuchukua hatua kali; ikiwamo kuwatimua kazini na kuwafungulia mashtaka wote wanaiba mali za wananchi, nasi katika Pambazuko tunasisitiza kiongozi huyo wa nchi yetu kuchukua hatua kwa wote wanaomhujumu.

Kuiba mali ya umma ni dhambi kubwa mno, kwani inahusisha kudhulumu haki za idadi kubwa ya wananchi. Kuiba fedha za maendeleo maana yake ni kwamba mwizi huyo anakwamisha ujenzi wa barabara, anachelewesha kama siyo kuzuia kabisa ununuzi wa dawa katika hospitali na anakwamisha kuimarika kwa elimu ya watoto wetu.

Mwizi wa mali ya umma ni mbaya mno. Ni sawa kabisa na kuu watu kwa manufaa ya mtu binafsi na gharama za wengi.

Ndiyo maana katika nchi zingine, mwizi wa mali ya umma hupeua adhabu kubwa ikiwamo kunyongwa ili kuwa fundisho kwa watendaji wengine wenye tamaa ya kupata utajiri wa harakaharaka kwa mgongo wa fedha za maendeleo ya umma.

Pambazuko linamuomba Rais Samia sasa kuwa mkali zaidi kwa wezi wote wa mali ya umma na wale wanaotumia vibaya dhamana zao.

Sisi Pambazuko tuko tayari kumsaidia kwa njia tunazoweza ili kuifanya Tanzania ikome kuwa shamba la bibi.

KAZI IENDELEE



Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe (kushoto) pamoja na Katibu Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padre Charles Kitima. Viongozi hawa na wengine walialikwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu, Dodoma kwa ajili ya kushuhudia utiaji saini wa mikataba mitatu ya kuboresha na kuendesha sehemu ya Bandari ya Dar es Salaam. Hafla hiyo ilifanyika jana. (Picha na Ikulu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

NUKUU



KUSAFIRI ni darasa. Ni mwalimu mzuri wa kuyatambua maisha kupitia mazingira tofauti na watu wengine mbali na mazoea. Mwenye kusafiri hufikiri tofauti na kutumia mwanya wa maeneo mapya kupambanua changamoto zake alizozoea - Msemo maarufu wa Wachina.

Tangazo

Pambazuko

Changia Pambazuko liendelee

WATUMBE wa Bodi ya Uhariri, Mhariri Mkuu, wahariri, waandishi na watendaji wote wa gazeti la Pambazuko waneendelea kufuraha kusambaza habari, makala, safu, maoni, picha kwa miezi 15 bure kwa wasomaji wake.

Katika kipindi chote hicho cha kusambaza habari bila malipo, watendaji wa Pambazuko wamekuwa wakitumia fedha, muda, ujuzi na rasimali zingine kuhakikisha kila Jumatatu, gazeti hili linawafikia zaidi ya watu 500,000 duniani kote, bila malipo.

Ikumbukwe kwamba wasungumizi wa lugha adhimu ya Kiwahili duniani kote: wanalitumia gazeti hili siyo kwa kupata habari tu, bali hata kusambaza kwa wengine kujifunza lugha hiyo inayokua zaidi kwa sasa.

Katika kipindi cha uhai wa gazeti hili – miezi 15, mengi mazuri yamepatikana, mbali na kukua Kiwahili, kuhabarisha, kupaza maoni ya watu, lakini pia Pambazuko limeweza kusukuma watao uamuzi, hasa serikali kuchukua hatua kwenye baadhi ya mambo ambayo yameweka wazi kwa umma. Gazeti hili limesaidia kupeusha majanga, kuponya majeraha na zaidi sana, kuunganisha jamii na kuchochea umoja na kumharisha amani.

Pamoja na mafanikio hayo makubwa – na bado yanaendelea, uongozi wa Pambazuko umepokea mawazo kwamba gazeti hili lianze kuzwa, lakini haukubaliani na mawazo ya idadi kubwa ya wasomaji wake wanaopendekeza gazeti hivyo.

Lakini, uongozi huo umekubaliana na mawazo ya wachache kuruhusu umma kuanza kuchangia fedha kwa hizi ili kutoa mwanga kwa gazeti hili kuendelea kuifika umma bure.

Sasa basi, endapo utapata kuchangia maendeleo na uhai wa Pambazuko, tafadhali tumia namba hizi kwa ajili ya mchango wako wa fedha.

Unaweza kutuma mchango wako na kuhimiza wengine kufanya hivyo kwa kuanzia shilingi 1,000 na hakuna ukomo wa kiwango cha juu; chochote kinapokelewa kwa shukrani na hakika tutatambua mchango wako. Kwetu sisi, hutuna kilubwa wala kidogo; yote ni mchango na ina thamani sana ya "asante" kutoka kwetu.

Tuma mchango wako kutoka mtandao wovote wa simu yako ya mkononi - kwenda namba hii ya Lipa kwa TIGO na utafukia; 6214500, Pia unaweza kuchangia kupitia namba ya Mpesa: 0744 768 263

Ukituma mchango wako kupitia simu, hakikisha jina linaandika: **Pambazuko Gazeti.**

Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako – na wale wengine uliowaomba kuchangia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263.**



Endapo utapata changamoto katika kutuma mchango wako – na wale wengine uliowaomba kuchangia, tafadhali wasiliana nasi kwa namba hii na utahudumiwa kwa furaha; **0744 768 263.**

**Mhariri Mkuu,
Oktoba, 2023**

Makonda wa JPM vs Makonda wa Samia

Na Igo AI

EBHANA ehh – masalalee! Tai amejiinamia, anawaza na kupambanua ukweli wa msemu wa Kiswahili wa “usiyempenda kaja.”

Msemu huu umeingia kichwani mwa Tai baada ya kufuatilia kwa karibu taarifa ya Chama Cha Mapunduzi (CCM), iliyotolewa jana kwamba chama hicho tawala, kimempa ajira Paulo Makonda.

Makonda huyu aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Yule aliyekuwa anagusana mabega na kuingia Ikulu kama anavyotaka. Huu ni wakati ule wa uongozi wa John Pombe Magufuli (JPM).

Ndiyo, ni yeye yule ambaye anadaiwa na wananchi kadhaa kwamba alitumia madaraka yake vibaya. Kwamba alituhumiwa kwa hili na lile.

Ni yule aliyedaiwa eti kumzaba kibao mmoja wa mawaziri wakuu wastaafu. Hata hivyo, hili haijawahi kuwekwa wazi na waziri mkuu huyo, wala kukanushwa na Makonda mwenyewe, linabaki kuwa tuhuma tu.

Tai akakumbuka kwamba ni huyu Makonda ambaye Marekani ikambesha tuhuma nzito, kwamba alikuwa akishiriki katika mipango ya “kuzuia binadamu kula.”

Kwa tuhuma hizo kutoka taifa kubwa na lenye nguvu zaidi za kiuchumi na kijeshi duniani, likaamua kumnyima haki ya kutembelea nchi hiyo – kwamba asikanyage ardhi ya Marekani.

Kama haitoshi, Tai akakumbuka kwamba Marekani, haikumzuia Makonda peke yake, yaani hadi mke wake, Mary Felix Massenge naye akaingizwa kwenye “ban.”

Marekani bhana! Yaani ikadai kuwa Makonda anahusika kuminya haki za binadamu, haki ya uhuru wa kujiamulia mambo na usalama wa watu.

Ni huyu Makonda ambaye akajenga uadui na matajiri wengi wa Dar es Salaam ambao, kwa nguvu kubwa alizokuwa



Paulo Makonda.

nazo wakati huo, akadaiwa kuelekeza wakamatwe, waswekwe korokoroni, akiwatumu kuhusika na biashara na au matumizi ya dawa za kulevya.

Makonda hakukomea kwa matajiri tu, akaingilia hadi familia za marais wastaafu. Akalazimisha Polisi wawakamate watu aliokuwa na orodha yao na kuelekeza wapimwe mkojo; kwamba watafute “kila chembe ya dawa za kulevya katika miili yao ili awashughulikie.”

Tai akashtuka, akaona muda unaenda na anaendelea kuorodhesha tuhuma alizobebeshwa Makonda wakati wa utawala wake. Akataza jua na kuona linazama, akaamua bora awahi kiotani kwake akaendeleo kuziweka kwenye karatasi kubwa zaidi.

Alipofika kiotani mwake, Tai akachoka kuorodhesha, akaona heri aangalie yalipo mazuri ya Makonda; akashika kalamu na karatasi nyingine, akaanza, lakini akaacha, akasema amsubiri Makonda mpya ambaye sasa anaanza kuwa msemaji wa CCM.

Tai akapima nguvu zake kwa nafasi hiyo mpya, akajipa moyo kwamba, sasa amekuja Makonda mpya - wa Samia.

Akajisemea, Makonda yule wa JPM, aachwe apumzike.

Wasiliana na mtumishi wa Tai kwa namba hii: 0744 768 263

Habari

Rostam apeleka umeme Zambia

Na Mwandishi WETU,
Lusaka

MFANYABIASHARA maarufu nchini, Rostam Aziz, amezidi kupanua mawanda ya uwekezaji na sasa ameingia katika Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kupitia Zambia – anakopeleka umeme.

Akitumia kampuni yake ya Taifa Gas, mfiyabiashara huyo anafanya uwekezaji wa awali unaofikia dola za Marekani 100 milioni katika sekta ya uzalishaji umeme kwa kutumia gesi kwa kushirikiana na kampuni nyingine ya Zambia, Delta Marimba.

Taifa Gas na Delta Marimba zimeunda kampuni ya ubia, Taifa Marimba, ambayo imeshaanza uwekezaji wa kiasi hicho cha fedha kuzalisha megawati 100 za umeme katika eneo la Kasama kwa ajili ya kuuza nishati hiyo kwenye migodi ya madini.

Hii ni nchi ya pili kwa Rostam kuwekeza nje ya Tanzania katika miezi ya hivi karibuni. Mapema mwaka huu alifanya uwekezaji mkubwa nchini Kenya ambako anajenga kiwanda cha kuchakata gesi ya kupikia katika mji wa Mombasa.

Hatua ya Rostam kuingia Zambia imemfurahisha Rais wa nchi hiyo, Hakainde Hichelema ambaye amemhakikishia mfiyabiashara huyo kuwa serikali yake itatoa ushirikiano wote

atakaouhitaji ili kufanikisha uwekezaji huo.

“Haya ndio mambo ambayo Bara la Afrika linataka kuyasikia, kuwa kampuni kutoka nchi tofauti zinaungana pamoja kwa ajili ya kufanya uwekezaji mkubwa kwa manufaa ya nchi na watu wake,” alisema Hichelema wakati Rostam na ujumbe wake walipomtembelea Ikulu jijini Lusaka Ijumaa iliyopita.

Hivi sasa Zambia inakabiliwa na upungufu wa umeme kwani kwa muda mrefu imekuwa ikitegemea umeme unaozalishwa kwa vyanzo vya maji ambavyo vimeathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi.

“Sasa tumedhamiria kutafuta vyanzo vingine vya uzalishaji umeme na uamuzi huu wa Delta Marimba kutumia gesi kuzalisha umeme, unaendana na mikakati ambayo serikali yetu imepanga kuitekeleza, hivyo tunawaunga mkono,” alisema Rais Hichelema.

Viongozi hao ambao walifanya mazungumzo ya wazi kabla ya kuingia kwenye yale ya faragha, walikubaliana kuwa wakati umefika sasa kwa kampuni za Afrika kuunganisha nguvu ili kuweza kuwa na mitaji ya kutosha itakayoziwzesha kuzitumia malighafi nyingi zinazopatikana barani humu.

“Afrika ni bara linalotambulika kwa

inaendelea Uk. 7



Rais wa Zambia, Hakainde Hichelema (kulia) akizungumza na Rostam Aziz kuhusu asma yake ya kuwekeza katika nchi hiyo. Mazungumzo hayo yalifanyika Ikulu ya Zambia iliyoiko Jiji la Lusaka. (Picha kwa hisani).

Rostam apeleka umeme Zambia

Inatoka Uk. 6

kutoa malighafi kwa ajili ya nchi nyingine. Tuna uwezo wa kukomesha hilo kwa kuziwezesha kampuni zetu kuungana na kuwa na nguvu kubwa kiuchumi,” alisistiza Rais Hichelema.

Rais huyo alibainisha kuwa uamuzi wa Taifa Gas na Delta Marimba kuungana na kuwekeza nchini mwake ni uthibitisho kuwa panapokuwa na dhamira hakuna kinachoweza kukwamisha kampuni za Afrika kuingia ubia.

“Tunafurahi kuwa uwekezaji wenu wa awali mmeuelekeza kwenye uzalishaji wa umeme kwa ajili ya sekta ya madini. Kuongeza thamani katika sekta hii ni jambo muhimu sana kwani kutachochea maendeleo ya uchumi, kutengeneza nafasi za ajira, kuleta fursa za biashara na uwekezaji kati ya wazawa nchini Zambia na wenzao katika ukanda huu,” alisema Rais Hichelema na kuongeza:

“Tanzania na Zambia sina ushirikiano wa muda mrefu na wa kidugu, kibishara na kijamii. Uhusiano huu sasa inabidi upelekwe juu zaidi kwa kuingiza miradi mikubwa ya kiuchumi yenye thamani kubwa kwa ajili ya manufaa ya nchi zetu hizi.”

Kwa upande wake, Waziri wa Nishati wa Zambia, Mhandisi Peter Kapala, alisema anaamini mradi huo ambao unalenga kubadili mitambo inayozalisha umeme kwa kutumia dizeli na kuifanya itumie gesi, utasaidia upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa bei nafuu.

Alisema wizara yake imejiandaa kutoa ushirikiano utakaohitajika ili kuiwezesha kampuni hiyo ya Taifa Marimba kufikia malengo yake.

“Kufanikiwa kwa kampuni hii ni kufanikiwa kwa Zambia kwani tutajihakikishia ongezeko la umeme unaozalishwa nchini,” alisema.

Kwa upande wake, Rostam alisema wameamua kuingia ubia na kampuni ya Zambia na kuwekeza nchini humo kama njia moja ya kukuza na kuendeleza

ushirikiano wa kidugu na kihistoria baina ya Tanzania na Zambia.

Alisema pia kuwa ushirikiano huo unathibitisha kuwa suala la kampuni za kutoka nchi tofauti barabani Afrika zinaweza kushirikiana na kufanya mambo makubwa.

Alisemama kwa sasa wataanza na mradi huo wa kuzalisha megawati 100 lakini baadaye watanuua na kuzalisha umeme mwingi zaidi kwa kutumia nguvu za jua na upepo.

“Lakini pia mpango wetu ni kutanua uwekezaji wetu katika maeneo mengi nje ya uzalishaji wa umeme. Tunmeamua kufanya hivi kwa sababu tumeona fursa nyingi za kuwekeza hapa,” alisema Rostam.

Mfanyabiashara huyo alisema kampuni ya Taifa Marimba imejipanga kuwa balozi mzuri wa kuitangaza Zambia kama nchi yenye vivutio vingi vya uwekezaji.

“Sisi tumeonyesha mfano kwa kuungana. Tunataka tuitumie kampuni hii kama mfano kuzishawishi kampuni nyingine za Afrika kuunganisha nguvu na kufanya kazi pamoja, tunaamini Kuwa iwapo tutaungana tutakuwa na nguvu ya kufanya mambo mengi,” alisisitiza.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Delta Marimba, Padmore Muleya, alisema kazi ya upembuzi wa awali wa mradi huo inaendelea vyema na malengo ni kuhakikisha kuwa uzalishaji wa umeme unaanza katika kipindi cha miezi 24 ijayo.

“Tunashukuru kuwa Serikali ya Zambia inaunga mkono uwekezaji wetu kwa sababu unaendana na malengo ya kuhakikisha uzalishaji wa umeme unaongezeka kutoka katika vyanzo mbalimbali,” alisema.

Alisema hatua ya Delta Marimba kuingia ubia na Taifa Gas ili kuzalisha umeme inaonyesha dhamira ya kampuni hiyo kuunga mkono juhudi za serikali katika eneo la uzalishaji umeme kutoka vyanzo mbadala.

Habari

Deni la taifa Sh. trilioni 1.7 'layeyuka'

Na Mwandishi WETU

WAKATI baadhi ya nchi zikilalamika kutokana na kuimarika kwa dola ya Marekani na kuzifanya sarafu zao kuwa dhaifu, hali ni tofauti kidogo kwa Tanzania ambayo imenufaika na hali hiyo.

Kiasi cha Shilingi trilioni 1.778 kimeyeyuka katika deni la taifa katika kipindi kinachoshia Agosti 2023 kutokana na kuimarika kwa sarafu ya dola ya Marekani, Benki Kuu (BoT) imesema.

Hii ni kwa sababu kiasi kikubwa cha deni la Tanzania, hasa deni la nje, lipo katika sarafu za dola ya Marekani, Paundi ya Uingereza na Euro ya Ulaya.

Taarifa ya BoT inaeleza kuwa kuimarika kwa dola ya Marekani na kushuka kwa thamani ya Paundi na Euro kunayafanya madeni ya Tanzania ambayo yapo kwa sarafu hizo nayo kusinyaa. Na hii ndio faida ambayo Tanzania imeipata bila kutarajia au kupanga.

Ripoti ya hali ya uchumi kwa kila mwezi inayoangalia kipindi cha Agosti imebaini kupungua kwa kiasi cha deni la taifa kwa kiasi cha dola za Marekani bilioni 728.1 (trilioni 1.778/-) na kufikia dola za Marekani bilioni 40,574.6 mwishoni mwa mwezi Agosti.

Kwa mujibu wa BoT, deni hilo limepungua siyo kwa sababu limelipwa kiuhalisia, bali ni kutokana na mabadiliko ya viwango vya kubadilishana fedha baina ya sarafu ya dola na sarafu nyingine duniani.

BoT inabainisha katika ripoti hiyo kuwa mabadiliko hayo yalisababisha kumarika kwa sarafu ya dola dhidi ya sarafu nyingine duniani na hivyo kuinufasha Tanzania licha ya sarafu yake, yaani shilingi, nayo kuzidi kushuka thamani kulinganisha na dola ya Marekani.

Kwa kiasi kikubwa deni lililopungua ni deni la nje ambalo linaunda asilimia 70.5 ya deni lote la nchi.



Gavana wa Benki Kuu - Emmanuel Tutuba

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa mwishoni mwa Agosti, deni la nje lilikuwa ni kiasi cha dola za Marekani milioni 28,615.4, likiwa limepungua kwa dola milioni 725.8 kutoka kiwango cha mwezi uliotangulia.

“Kupungua huko kwa deni kwa kiasi kikubwa kulitokana na mabadiliko ya thamani ya kubadilisha fedha. Kuimarika kwa thamani ya sarafu ya dola ya Marekani dhidi ya sarafu nyingine zilizomo katika deni. Kiasi cha deni kilicholipwa katika mwezi huo ni dola milioni 74.4 tu,” inasomeka sehemu ya ripoti hiyo ya BoT.

Hali hiyo imejitokeza wakati ambapo uchumi wa Tanzania unaelezwa kukua vizuri hasa katika robo ya pili ya mwaka wa fedha.

Ripoti ya hali ya uchumi iliyotolewa hivi karibuni ya Shirika la Fedha Duniani (IMF), inaonyesha kuwa hali ya uchumi kwa Tanzania na nchi kadhaa, imeshaanza kudhibiti madhara ya kiuchumi yaliyotokana na madhara ya mlipuko wa Covid-19 na vita vya Urusi na Ukraine.



Mkulima wa korosho asaidiwe

Na Rashid MTAGALUKA

BODI ya Korosho Tanzania imeweka malengo kuongeza uzalishaji wa korosho ghafi kufikia tani 1,000,000 ifikapo 2030; kubangua asilimia 60 ya korosho hizo na kuwa na masoko ya uhakika na endelevu ya zao hilo na bidhaa zake ifikapo 2030.

Hili lilibainika wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Korosho uliofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam na kufunguliwa na Makamu wa Rais, Dkt Philip Mpango.

Hata hivyo, mkutano huo licha ya kutangaza fursa za uwekezaji zilizoko kwenye zao la korosho kuanzia shambani na kuimarika kwa masoko kwa kufungua masoko ya korosho na bidhaa zake ndani na nje ya nchi, hakukutangazwa kuanza rasmi kwa msimu wa zao hilo la biashara mwaka huu.

Wananchi wengi walitega masikio yao kwenye mkutano huo kwamba, huenda serikali ingetangaza kufunguliwa kwa msimu mpya wa ununuzi wa zao hilo ili shida, dhiki na unyonge walionao wakulima uondoke.

Sasa kwa ukimya huu, kuna haja gani viongozi wetu mara kadhaa kutoa maagizo yaliyojaa vitisho kwa wakulima hawa masikini ambao kwa mwaka nzima neema yao ni ndani ya miezi mitatu ya msimu wa korosho?

Kwa kumbukumbu zangu hakuna ngazi ya uongozi wa serikali hapa nchini ambayo haijawahi kuwatisha wakulima wa korosho kuacha kuuza korosho zao kwa wanunuzi wanaotumia bakuli, maarufu kangomba, wakidai wananyonywa.

Kwa mfano, tumewahi kumsikia aliyekuwa Waziri wa Kilimo Profesa Adolf Mkenda akionya vitendo vya wakulima kukubali kuuza korosho kwa



makangomba akidai wanapoteza haki yao kwa kuwa kipimo hicho siyo halali.

Naye aliyewahi kuwa Mkuu wa mkoa wa Lindi Godfrey Zambi enzi zake alipiga marufuku kutumia kipimo kinachotumiwa na baadhi ya wanunuzi wa mazao katika mkoa huo.

Spingani na maono ya viongozi hao wa serikali kuhusu nia yao njema kwa mkulima wa korosho, hoja yangu ni je, matamko hayo ya kumtaka mkulima asiuze korosho zake kwa Kangomba yanatatuaje shida yake kipindi hicho?

Nani katika viongozi - iwe wa serikali au hata wa bodi ya zao hilo anayeweza kuvumilia njaa kwa muda wa miezi mitatu tu ikitokea kuna changamoto ya kuchelewa kwa mshahara?

Naomba isidhaniwe kuwa, lengo langu ni kuwatetea hao walanguzi wanaotumia shida za wakulima kujinufaisha kwa kipimo hicho kinachoeleza kinawapunja.

Hoja kuu hapa siyo wakulima wote wanaouza korosho zao kwa kangomba wanaridhia kufanya hivyo lah, bali changamoto za kimaisha na hasa ikizingatiwa wananchi wengi hawana shughuli nyingine zinazowaingizia kipato zaidi ya kusubiria korosho.

Lakini, serikali ikitaka kutatua matatizo ya mkulima kwa mabavu huku ikiwekeza katika kutoa maagizo mazito kila kukicha, kamwe siyo afya.

Mwandishi anapatikana kwa simu 0784 438 546/mtagaluka@gmail.com

Habari**Hatimaye DP World waanza kazi**

Na Scovya MANASE

SASA ni rasmi. Kwamba uchumi wa Tanzania utakua zaidi kwa kuwa kichocheo cha kukusanya mapato; Bandari ya Dar es Salaam, inakuwa ya kisasa na yenye ufanisi mkubwa, Pambazuko linaeleza.

Maboresho yanayokwenda kufanywa katika bandari hiyo kubwa Tanzania ni pamoja na kuongezwa kwa ukubwa wa magati; kuweka vifaa vya kisasa vya kupakia na kupakua shehena; kuweka mifumo inayosomana katika kutekeleza majukumu; na zaidi sana, kuwepo kwa watalaamu wa watendaji wenye uzoefu mkubwa katika uendeshaji wa shughuli za bandari.

Wanaofanya uwekezaji mkubwa wa maboresho ya bandari hiyo ni Kampuni ya DP World ya Dubai, ambayo jana imesaini mikataba mitatu ya awali na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

Hafu ya kutia saini mikataba hiyo mitatu ilifanyika Ikulu, Dodoma jana – Oktoba 22, mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan na Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa DP World, Sultan Ahmed bin Sulayem.

Mikataba hiyo mitatu iliyotiwa saini ni Mikataba wa Nchi Mwenyeji (HGA); Mikataba ya Ukodishaji; na Uendeshaji wa gati nambari nne hadi saba katika Bandari ya Dar es Salaam.

Katika uwekezaji huo, DP World imepanga kuwekeza kiasi cha dola za Marekani milioni 250 (sawa na Shilingi bilioni 625) katika kipindi cha miaka mitano ya mwanzo, huko kiasi kinachotarajiwa kuboresha sehemu mahsusi ya bandari hiyo kufikia dola bilioni moja (sawa na Shilingi trilion 2.5).

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA),



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TPA, Balozi Ernest Mangu akipongezana na Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya DP World ya Dubai, Sultan Ahmed bin Sulayem mara baada ya kusaini Mikataba wa Uendeshaji wa Gati namba 4 mpaka 7 za Bandari ya Dar es Salaam. (Picha na Ikulu).

Plasduce Mbossa amesema mikataba utahusisha baadhi ya magati ya Bandari ya Dar es Salaam na siyo maeneo yote ya Bandari ya Dar es Salaam na mikataba hii haihusishi bandari nyingine za mwambao na maziwa.

“Mtaba huu una ukomo wa miaka 30 na utakuwa ukirejewa kila baada ya miaka 5, ikiwa ni pamoja na kurejea mpango wa uwekezaji,” amesema Mbossa.

Mbossa amesema pia kutakuwa na kampuni ya uendeshaji ambayo TPA itamiliki hisa; kuwekwa kwa viwango vya utendaji, ambazo mwekezaji anapaswa kuvifikia.

Mtendaji huyo mkuu wa TPA amesema kuwa wafanyakazi wa mamlaka hiyo wamepewa nafasi ya kuchagua kubaki kwa mwajiri wao wa sasa au kuamua kuhamia kwa mwekezaji.

“Jukumu la ulinzi na usalama katika eneo lote la bandari na yaliyokodishwa kwa Kampuni DP World yataendelea kubaki serikalini; mwekezaji atalipa kodi na tozo zote za serikali kwa kuzingia sheria za Tanzania,” amesema.

Amesema sheria za Tanzania zitatumika katika utekezaji wa mikataba hii ikiwa ni pamoja na kutoa

Hatimaye DP World waanza kazi

Inatoka Uk. 10

fursa za Watanzania kushiriki katika uwekezaji huu kupitia vifungu vya sheria vinavyolinda maudhui ya ndani ya nchi ni haki ya serikali kujiondoa katika mikataba hiyo imezingatiwa.

Mbossa amesema uwekezaji huo utakuwa na manufaa kwa serikali, ikiwemo ongezeko la ufanisi kwa huduma zitakazotolewa kwa meli na shehena hali itakayovutia meli nyingi zaidi na shehena kubwa ya mzigo itakayohudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kushuhudia utiaji saini wa mikataba hiyo, Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan amesema kuwa hatua hii inafikiwa baada ya kufanya uchambuzi wa kina ikiwemo maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Watanzania wa kada mbalimbali.

Mara baada ya kuvuja kwa mkataba wa awali wa uwekezaji (IGA) huo wa DP World, watu wa kada mbalimbali; viongozi wa dini, wanasheria, wanazuoni na wengine, waliibuka na mawazo ya kuomba kuboresha kwa baadhi ya vifungu ili Tanzania iweze kunufaika kwa uwekezaji huo.

“Serikali kwa upande wake ilisikiliza michango na maoni mbalimbali yaliyotolewa na Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), vyama vya siasa, asasi za kiraia, wanaharakati huru na vyombo vya habari,” alisema Rais Samia.

Rais Samia pia alieleza kwamba serikali anayoongoza ilipitia maoni ya wananchi katika mitandao ya kijamii; Instagram, X, Jamii Forums, Facebook na mingine.

Zaidi pia, Rais Samia amesema serikali ilisikiliza na kufanyia kazi baadhi ya mapendekezo ya viongozi wa dini katika kuboresha mkataba huo.

Rais Samia amesema uwekezaji huo mkubwa unaotekelezwa na Kampuni ya DP World utabadilisha utendaji wa

Bandari ya Dar es Salam na kuiwezesha kuchangia zaidi katika pato la Taifa.

Moja ya faida kubwa ya uwekezaji huo imeelezwa kuwa kuongezeka kwa makusanyo kodi, ushuru wa firodha na tozo mbalimbali ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) itaweza kukusanya Shilingi trilioni 26.7 kufikia mwaka 2032 tofauti na sasa ambapo mamlaka hiyo inakusanya Shilingi trilioni 7.8 kwa mwaka.

Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya DP World, Sultan Ahmed bin Sulayem amesema katika miaka mitano ya mwanzo DP World itaweza katika kuboresha miundombinu ya kushughulikia mizigo kwa haraka ili kuondoa kero ya ucheleweshaji wa mizigo unaoikabili bandari hiyo.

Benki ya Dunia (WB) imekuwa ikieleza kwamba endapo Tanzania itawezekeza kwemye bandari ya Dar es Salaam, pekee inaweza kuchangia zaidi ya nusu ya mapato ya nchi ikiwa “mambo makubwa na ya kisasa” yatafanyika.

Mambo makubwa yanayozungumzwa na Benki ya Dunia ni uwekezaji wa miundombinu, uongozi wenye kukuza tija, kutafuta masoko zaidi, usalama wa mali na mizigo, kutumika kwa teknolojia na uimara wa kuendesha bandari kitaalamu.

Mbali na Benki ya Dunia kueleza namna bandari za Tanzania zinavyoweza kung’arisha uchumi wa nchi hiyo, Aprili 15, 2015, Rais wa Rwanda, Paul Kagame akiwa na ziara nchini, alisikika akinong’ona na Rais Jakaya Kikwete, kwamba akipewa kuendesha Bandari ya Dar es Salaam kwa miaka 10 au zaidi, atabadili historia ya makusanyo ya kodi.

Sifa zote hizi zinabeba umuhimu na kuwepo manufaa makubwa ya bandari za Tanzania katika kukuza uchumi wake na ustawi wa watu wake, hata hivyo,

Mtazamo

Tanzania na kizungumkuti cha haki za binadamu

Na Jabir IDRISSA

NIMESOMA toleo la Jumamosi la gazeti la Uhuru linalomiliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) likiwa na cha habari: Tanzania kinara wa haki za binadamu.

Kwamba taifa hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liko vizuri, linajitahidi kulinda haki za binadamu na kutekelezwa kama isemavyo mikataba ya kimataifa ambayo serikali yetu imeiridhia kwa kuisaini.

Kwamba jitihada hizo ni pamoja na kuboresha hali na upatikanaji wa haki za binadamu zikiwemo usawa mbele ya sheria, afya, elimu, maji, mazingira safi, uhuru wa kutoa maoni, wa kuabudu, haki ya ajira, ya kumiliki mali na uhuru wa vyombo vya habari.

Msimamo wa taifa letu, kupitia serikali ambayo tunaambiwa imesajili vituo 210 vya redio, vituo 56 vya televisheni, magazeti 288 na mitandao ya kijamii mingi zikiwemo televisheni za online.

Isitoshe, Tanzania imeimarisha demokrasia, haki za wanawake, watoto na watu wenye ulemavu “kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.” Kuwa hizo haki kuhakikishwa kwake huzingatia uwiano wa wanawake na wanaume, na watu wenye ulemavu wakihusika.

Msimamo huu umewasilishwa na Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, katika ufunguzi wa Mkutano wa 77 wa Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, uliofanyika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), jijini Arusha wiki iliyopita.

Dkt. Mwinyi akasema ni vyema nchi za Afrika zikachukua hatua kukabiliana na matatizo yanayozorotisha upatikanaji wa haki za binadamu, huku akitilia mkazo



Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi,

kuwa wahanga wakubwa wa ukosefu wa haki hizo, ni wanawake na watoto.

Kuhusu Tanzania, Dkt. Mwinyi alisema inatambua hali hiyo na kuendeleza jitihada za kutatua migogoro mbalimbali na kutekeleza Tamko la Dar es Salaam juu ya Amani, Usalama, Demokrasia na Maendeleo kwa ukanda wa nchi za maziwa makuu.

Hofu kuu nayoiona hapa ni uongozi kutangaza msimamo huu katikati ya wingu zito la kuwepo madai ya kuzivunja haki za msingi za binadamu.

Unatumia takwimu za usajili vituo vya televisheni, redio na magazeti kuonesha eti ni uthibitisho wa serikali kuheshimu uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza.

Ukatumia idadi ya vyama vya siasa vilivyosajiliwa, Tanzania tuseme vipa 19, na kuonesha serikali imepanua wigo wa demokrasia ya vyama vingi. Huelezi vikwazo vya utendajikazi wa vyama hivi, wala hujali kuwa baadhi yake vipo vinavyoendeshwa kisanii kukidhi maslahi binafasi, bali pia na matakwa ya chama kile kinachoshika dola.

Huelezi kamwe namna dola inavyovihujumu vyama hivi, tena kwa

Inaendelea Uk. 13

Tanzania na kizungumkuti cha haki za binadamu

Inatoka Uk. 12

kutumia fedha za walipakodi. Na husemi vilevile kwamba kiu ya chama tawala ni kutwaa kila kitu wakati wa uchaguzi, hivyo fedha kutumika kusimamia hiyo kwa nguvu zote. Ikibidi wapigwe na wauliwe, chama kichukuwe vyote.

Kwenye hilo, umma unashuhudia kwa njia mbalimbali, mkakati wa kudhibiti kila mtu, na mwisho wa siku kukuta vyombo vya kutunga sheria na kuzisimamia serikali vikijengwa na wao peke yao.

Kwenye eneo la uhuru wa kutoa maoni, ni nani asiyejua shida wanazokumbana nazo waandishi wa habari wanapotaka taarifa maofisini; iwe wizara, idara au shirika kuhusu masuala yanayogusa maslahi ya watu ikiwemo kucheki matumizi ya raslimaliwatu na fedha?

Waandishi kutakiwa waandike maswali, kufuatilia kwa simu kama yamejibiwa na kulazimika kwenda na kurudi; bado majibu yasipatikane kwa wakati muafaka.

Rais wa Zanzibar mwenyewe amechukua hatua gani, zaidi ya kukumbusha tena na tena viongozi walio chini yake wasifiche taarifa kwa waandishi wa habari?

Kwa kweli mwenendo halisi unaonesha serikali inachekelea kupokea maombi mengi na kusajili tu kwa nia ya kuongeza mapato kwenye mfuko wake. Haina cha kufanya kuvisaidia vyombo kujijenga kiuchumi kwa kuwa vyeneyewe vinalipa kodi na vinatoa ajira kwa jamii.

Kuthibitisha hali ya utaji taarifa ni tete Zanzibar, leo tunaona na yeye rais, aliyeanzisha utaratibu wa kukutana na waandishi wa habari angalau kila mwisho wa mwezi, kama vile amechoka, na kususa. Tangu mwezi Julai hajaita kikao.

Serikali inatunga sheria kali, kanuni katili za maudhui ya utangazaji kiasi



cha kutishia uhuru wa haki yenyewe ya umma kupata taarifa. Haki ya kujua. Inaonekana dhahiri shahir, ni shauku ya serikali kuwapa taarifa wananchi ni zawadi si wajibu wake.

Zaidi ya miaka kumi Zanzibar inahitajia sheria rafiki ya huduma kwa vyombo vya habari, na licha ya harakati na mashauriano ya mara kwa mara, vyombo vya habari na washirika wao, wangali wanasubiri kuona muswada unasomwa kwenye Baraza la Wawakilishi.

Usalama wa raia: Fikiria unapokuwa na kikosi kinachotunzwa kwa ajili ya kupiga na kujeruhi watu kwa njia ya kuwakata viungo vyao, kwa kisingizio kuwa ni vibaka, waweza kujinasibu unajali haki za binadamu?

Haki ya kuchagua/kuchaguliwa: Sawa inatolewa kila miaka mitano kwa mujibu wa Katiba. Lakini je, unazihishemu kura zao na kwamba zeneyewe ndio ziachwe kuamua nani awe kiongozi? Au huu mtindo uliozoeleka wa chama tawala kuvitumia vyombo vya ulinzi na usalama kujitwalia madaraka ndio mpango mzima?

Ya nini basi Katiba; na ikaelekeza kuwa mamlaka yote ya nchi hutoka kwa wananchi? Ni kujifunza kuwa umma useme "huyu hapana, bali yule ndo awe."

Ni kujidanganya, ukadanganya wananchi na kudanganya ulimwengu ambao kwa bahati nzuri u ajua kila kinachoendelea kutokea nchini kwako.

Habari

Hatimaye DP World waanza kazi**Inatoka Uk. 11**

kukosekana kwa ubunifu wa watendaji wa bandari hizo, na sababu zingine, kumezifanya kuchangia kiasi kidogo cha kodi katika Hazina.

Ili kuweka hesabu rahisi na kutambua wingi wa mapato yanayoweza kupatikana kwenye sekta ya bandari pekee, ikiwa uwekezaji na umakini utawekwa, ndani ya siku 100 - kuanzia Aprili Mosi hadi Juni, 2021 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) ilikusanya Sh. 236.8 kutoka Sh. 203 bilioni. Hii ni ongezeko la asilimia 14.

Mbarawa azungumza

Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa ameliambiwa Pambazuko kwamba kukwama kwa mchango mkubwa kwenye makusanyo ya kodi kwenye bandari kunatokana na ufinyu wa bajeti na kwamba serikali “inabanana kutimiza mahitaji mengi ya nchi,” hivyo kuhitaji mwekezaji makini katika kuendesha bandari.

Anasema bandari, hasa ya Dar es Salaam, imekuwa ikifanya vizuri, lakini inaweza kufanya vizuri zaidi endapo kutafanyika uwekezaji mkubwa na makini kwa kupata kampuni yenye uzoefu, mtaji, ujuzi na weledi katika kuendesha biashara ya bandari.

Prof. Mbarawa anasisitiza kwamba katika mazingira ya sasa, serikali nyingi duniani, zinajiondoka katika uendeshaji na kuweka fedha nyingi katika miradi ya kiuchumi, na kutoa nafasi ya ushirikiano na sekta binafsi.

DP World wafika

Katika kutafuta mwekezaji makini baada ya kumalizika kwa muda wa Kampuni ya TICTs iliyokuwa ikiendesha sehemu ya Bandari ya Dar es Salaam, Serikali ya Tanzania ilianza mchakato wa kupata mwekezaji ambaye ana mtaji wa kutosha, ujuzi, weledi wa kuendesha shughuli na kuongoza bandari.

Mchakato huo hatimaye ukapata kampuni inayomilikiwa na Utawala wa Kifalme wa Dubai ya DP World ambayo imekuwa ikifanya shughuli za kuendesha bandari kwa ufanisi mkubwa kwenye nchi za Ulaya, Amerika na Afrika.

Katika eneo la kukuza uchumi, serikali za Dubai na Tanzania zilijadili na kuafikiana kuwepo kwa makubaliano ya awali baina ya nchi hizo (IGA) ambayo yatairuhusu Kampuni ya DP World kuendesha bandari kadhaa za Tanzania kwa njia ya kukodisha kwa muda maalum ambao utawekwa kwenye mkataba mahsusi wa kibiashara kwa nchi hizo (HGA). Tayari Bunge la Tanzania limerishia kuanza kwa mchakato wa kufunga mkataba baina ya nchi hizo (HGA) ili kuruhusu DP World kuanza shughuli za kusimamia na kuendesha bandari za Tanzania.

Pia uwekezaji wa DP World utapunguza muda wa meli kukaa nangani kutoka siku tano kwa sasa hadi saa 24 kutokana na kuwekeza katika miundombinu ya kisasa.

Hatua hii itaongeza idadi ya meli zitakazotia nanga Bandari ya Dar es Salaam kutoka meli 1,569 zilizohudumiwa mwaka 2021/22 mpaka kufikia takriban meli 2,950 ifikapo mwaka 2032/33.

Pia ujio wa kampuni hiyo ya Dubai utapunguza muda wa kushusha makontena kutoka siku 4.5 mpaka siku 2 na kupunguza muda wa uondoshaji mizigo kutoka saa 12 mpaka saa moja kutokana na uboreshaji wa mifumo ya Tehama.

Kuingia kwa Dp World kutapunguza gharama ya usafirishaji wa shehena kutoka nchi za nje kwenda nchi za jirani, kwa mfano kutoka dola za Marekani 12,000 mpaka kati ya dola 6,000 na 7,000 kwa kontena linalokwenda nchi za Malawi, Zambia au Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Burundi, Rwanda na nchi zingine jirani.

Mtazamo wa TPA kwa DP World

Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa katika hafla ya utiaji saini wa mikataba mahsusi ya uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam. Mikataba hii ni kati ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya DP World ya Dubai. Hafla hiyo ilifanyika jana – Oktoba 22, jijini Dodoma.

Kwa niaba ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), naomba niongee machache kuhusiana na tukio hili kubwa na la kihistoria ambalo linaenda kufanya mageuzi makubwa yenye mchango chanya katika huduma za Bandari nchini.

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana leo hapa kwa madhumuni ya kushuhudia utiaji saini Mikataba Mitatu ya Uwekezaji na Uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Naomba kwa namna ya pekee nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi pamoja na Serikali yako ya Awamu ya Sita unayoiongoza kwa dhamira ya dhati katika kuhakikisha kuwa huduma za Sekta ya Uchukuzi hususani zile za Bandari zinatolewa katika viwango shindani kimataifa kwa kuimarisha uendeshaji wa Bandari zetu.

Dhamira hii ya Serikali sasa inaongeza uwezo wa bandari zetu katika utoaji wa huduma kwa ufanisi, kupunguza gharama, kuinua uchumi ikiwa ni pamoja na ukuaji wa uwekezaji, biashara, ajira, mapato ya kodi na yasiyo ya kodi pamoja na kutumia ipasavyo fursa ya kijiografia ya nchi yetu katika kanda ya Afrika Mashariki na Kati kwa ujumla.

Bandari zetu zinaendeshwa katika hali ya ushindani kama zilizvya bandari nyingine duniani. Mazingira hayo



Plasduce Mbossa

yanachagizwa na mabadiliko ya ukuaji wa sekta ya usafirishaji majini, teknolojia na ukuaji wa uchumi. Hivyo, TPA kama Taasisi iliyokasimishwa jukumu la umiliki, uendeshaji, uendelezaji na usimamizi wa Bandari nchini ina jukumu la kutoa huduma sambamba na kasi ya mabadiliko hayo.

Katika kuendana na kasi ya mabadiliko hayo, moja ya mikakati ambayo imebainishwa katika Mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Bandari Tanzania wa mwaka 2009 ambao ulifanyiwa marejeo mwaka 2022, umetoa mapendekezo kwa Serikali kuhusu namna ambayo inaweza kufikia azma yake ya TPA kuwa Mmiliki na/au Mwendelezaji wa bandari nchini na kukasimisha shughuli za uendeshaji kwa Sekta Binafsi ili kuongeza ufanisi wa Bandari za Tanzania.

Pamoja na kuchukua hatua mbalimbali za maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam, bado ufanisi katika utoaji huduma za bandari haujafikia viwango vinavyotakiwa kimataifa.

Hali ya sasa ya utendaji wa Bandari

Taarifa

Mtazamo wa TPA kwa DP World

Inatoka Uk. 15

ya Dar es Salaam imeendelea kuwa ya kiwango cha chini ikilinganishwa na bandari shindani kikanda. Kwa mfano, meli nyingi husubiri nangani kwa muda mrefu kabla ya kuhudumiwa.

Leo hii, kuna meli 30 zilizofika bandarini (nangani) zikisubiri kuingia bandarini kushusha mizigo wakati zile zinaazohudumiwa gatini ni jumla la meli 11.

Wastani wa meli kusubiri nangani kwa Bandari ya Dar es salaam ni siku 5 ikilinganishwa na siku 1.25 kwa Bandari ya Mombasa na siku 1.6 kwa Bandari ya Durban.

Ufanisi huu mdogo wa Bandari ya Dar es Salaam umetokana na changamoto mbalimbali zikiwemo: kukosekana kwa mifumo ya kisasa ya Tehama ambayo haiwezi kusomana; kutokuwepo kwa maeneo ya kutosha ndani na nje ya bandari kwa ajili ya kuhifadhi shehena ya mizigo pamoja na uchache wa magati au maegesho ya meli.

Na kukosekana kwa mitambo ya kutosha na ya kisasa ya kuhudumia shehena ambayo teknolojia yake inabadilika mara kwa mara na ina gharama kubwa ya uwekezaji na uendeshaji.

Athari za kutokuwa na ufanisi katika Bandari ya Dar es Salaam ni pamoja na: meli kusubiri muda mrefu nangani ambako kunasababisha kuongezeka kwa gharama ya kutumia bandari ya Dar es Salaam, kwa mfano gharama za meli kusubiri nangani kwa siku moja ni takriban Dola za Marekani 25,000, sawa na takriban Shilingi milioni 58 kwa siku; meli kutumia muda mrefu kupakia na kupakua shehena gatini kwa wastani wa siku 5 ikilinganishwa na siku 1 inayokubalika kimataifa; meli kubwa kutokuja katika bandari ya Dar es Salaam

kutokana na kuchukua muda mrefu kuhudumiwa.

Hali hii husababisha bandari yetu kuwa bandari inayolishwa shehena na bandari nyingine (feeder port) na hivyo kuongeza gharama ya kutumia bandari hiyo na kuikoshesha nchi mapato ambayo yangeweza kutumika katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati nchini ambayo ingesaidia kukuza uchumi na kuboresha huduma za wananchi.

Pia, hali hii ya kukosekana kwa ufanisi inaongeza gharama katika mnyororo mzima wa usafirishaji (total route costs) kutoka nje ya nchi, kupitia katika bandari yetu kwenda nchi za jirani zinazotumia bandari hiyo ya Dar es Salaam.

Kwa mfano, gharama ya kusafirisha kasha moja kutoka nje ya nchi (on transit) kwenda nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zinafikia takriban Dola za Marekani 12,000. Hii ni gharama kubwa sana ikilinganishwa na Bandari shindani za Mombasa, Beira, Maputo na Durban ambazo ni wastani wa nusu ambazo zinatumika kwa kutumia bandari ya Dar es Salaam.

Gharama za usafirishaji kwa mizigo ya ndani ni takribani Dola za Marekani 6,000 kwa kasha ambazo zinapelekwa kwa mlaji wa mwisho ambaye ni mwananchi wa kawaida. Gharama za kupitisha mzigo kama huo kwa bandari jirani ya Mombasa ni takribani Dola za Marekani kati ya 3,500 hadi 4,000.

Kwa kutambua kuwa Serikali pekee haitaweza kutatua changamoto zilizopo kwenye Bandari ya Dar es Salaam, kuanzia miaka ya 2000, Serikali ilianza kushirikisha sekta binafsi na iliingia mkataba wa upangaji na uendeshaji (lease and concession agreement) na Kampuni ya Kimataifa ya Uendeshaji wa Vitengo vya Makasha, Hutchison ya Hong-Kong

Mtazamo wa TPA kwa DP World

Inatoka Uk. 16

China kupitia Kampuni ya TICTS.

Mkataba huo ulidumu kwa miaka ishirini na mbili (22) kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2022 na kampuni hiyo ya TICTS ilipewa haki ya kipekee ya kuendesha shughuli za kuhudumia makasha katika gati namba 8 hadi 11 za Bandari ya Dar es Salaam.

Wakati huo huo TPA iliendelea kuendesha na kuhudumia maeneo mengine ya Bandari hiyo ya gati namba 0 hadi 7 pamoja na magati ya mafuta ya KOJ na SBM.

Kampuni nyingi zimekuwa zikionesha nia ya kuendesha bandari ya Dar es Salaam lakini TPA iliingia makubaliano na Kampuni ya DP World kutokana na uzoefu wake katika uendeshaji wa shughuli za bandari barani Afrika, Asia, Ulaya na Amerika ya Kaskazini na Kusini. Kampuni hiyo pia, ina utaalumu wa kuchagiza mnyororo mzima wa usafirishaji (end to end total logistics chain solution) kutoka maeneo ambayo bidhaa zinatoka mpaka kufika kwa Walaji.

Pia, uendeshaji wa maeneo maalum ya kiuchumi (special economic zones) karibu na bandari, usafirishaji baharini na nchi kavu (kupitia njia ya reli), uwekezaji mkubwa katika maeneo mbalimbali ambayo imewekeza pamoja na kuajiri Wazawa katika maeneo hayo.

Kwa upande wa makampuni mengine ambayo yaliwasilisha mapendekezo yao yalioneshia nia ya kuwekeza bandarini pekee na sio kuchagiza mnyororo mzima wa usafirishaji na kutafuta masoko ya kimkakati katika eneo la usafirishaji wa shehena ya mizigo.

Pia, baadhi ya makampuni hayo hayana uzoefu wa kuendesha shughuli za bandari barani Afrika wakati Kampuni



DP World kasini

ya DP World inaendesha takriban bandari sita (6) barani Afrika na bandari zaidi ya 68 duniani kote kwa ufanisi mkubwa.

Katika kutekeleza mikakati ya Serikali ya kuimarisha shughuli za bandari ya Dar es Salaam; muda mfupi ujao utashuhudia utiaji saini wa mikataba mitatu (3) ya uwekezaji na uendeshaji wa bandari ya Dar es Salaam ambayo ni: Mkataba wa Nchi Mwenyeji, Mikataba ya Ukodishaji na Uendeshaji wa Gati Namba 4 hadi 7 za bandari ya Dar es Salaam.

Aidha, Gati Namba 0 hadi 3 za bandari ya Dar es Salaam zitatumiwa kwa pamoja baina ya Kampuni ya DP World na Serikali kupitia TPA kwa ajili ya shughuli zingine za kibiashara na Serikali.

Naomba kuisisitiza kwamba, mikataba hii haihusishi eneo lote la Bandari ya Dar es Salaam na bandari nyingine za Tanzania.

Naomba kukutaarifu kwamba, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari

Taarifa

Mtazamo wa TPA kwa DP World

Inatoka Uk. 17

Tanzania imeanza mchakato wa kumpata mwekezaji wa ndani au wa nje kwa ajili ya kuendesha Gati Namba 8 hadi 11.

Katika Mikataba hiyo mitatu (3), Serikali itakuwa ikipokea ada na tozo kutoka kwa Kampuni ya DP World ambazo zitaongeza mapato yake na kupunguza gharama za uendeshaji.

Hapo awali, Serikali ilikuwa inatumia takribani asilimia 90 ya mapato yaliyokusanywa katika uendeshaji wa maeneo hayo yaliyokodishwa na kubakiwa na asilimia 10 tu ya mapato yote. Hivyo, kutokana na Mikataba hii, Serikali itaweza kubaki na asilimia 60 ya mapato yote kutokana na gharama zote za uendeshaji kubakia kwa Kampuni ya DP World.

Aidha, faida ya mapato kwa Serikali itokanayo na maboresho ya huduma za bandari kupitia uwekezaji huu itaonekana moja kwa moja kwenye ukusanyaji wa ushuru wa forodha unaokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Mamlaka nyingine za Serikali zilizopewa majukumu kisheria kukusanya tozo, ushuru na ada mbalimbali kutoka katika shehena zitakazo hudumiwa na Bandari.

Ambapo tunatarajia mapato yanayokusanywa na TRA yataongeleka kutoka Shilingi Trilioni 7.8 za mwaka 2021/22 kwa mwaka hadi Shilingi Trilioni 26.7 kwa mwaka ifikapo mwaka 2032/33.

Ushirikishaji wa Sekta Binafsi katika uendeshaji wa Bandari sio kitu kipywa kwa Serikali na TPA lakini uwekezaji huu utakaenda kushuhudia utiaji sainei wa Mikataba ni wa aina yake ambao pamoja na masuala mengine ya kitaalam yaliyozingatwiwa.

Umezingatia changamoto ambazo

Serikali kupitia TPA ilizipata kupitia uwekezaji uliofanywa na kampuni ya TICTS ambayo muda wa mkataba wake ulikoma tarehe 31 Desemba 2022 pamoja na maoni mbalimbali ya wananchi.

Kama nilivyoeleza, uwekezaji huu umezingatia vitu vingi ndani yake kwa maslahi mapana ya nchi ikiwemo:

Mikataba kuhusisha baadhi ya magati ya Bandari ya Dar es Salaam na sio maeneo yote ya Bandari ya Dar es Salaam na mikataba hii haihusishi bandari nyingine za mwambao na maziwa;

Mkataba huu una ukomo wa miaka 30 na utakuwa ukirejewa kila baada ya miaka 5 ikiwa ni pamoja na kurejea mpango wa uwekezaji.

Kutakuwa na kampuni ya uendeshaji ambayo TPA itamiliki hisa; kuwekwa kwa viwango vya utendaji (key performance indicators) ambazo mwekezaji anapaswa kuvifikia;

Watumishi wa sasa wa TPA wamepeva nafasi ya kuchagua kubaki TPA au kuhamia kwa mwekezaji;

Jukumu la ulinzi na usalama katika eneo lote la bandari na yaliyokodishwa kwa Kampuni DP World yataendelea kubaki Serikalini;

Mwekezaji atalipa kodi na tozo zote za Serikali kwa kuzingua Sheria za Tanzania; Sheria za Tanzania zitatumika katika utekelezaji wa Mikataba hii,

Kutakuwa na fursa za watanzania kushiriki katika uwekezaji huu kupitia vifungu vya Sheria vinavyolinda maudhui ya ndani ya nchi (local contents), na

Haki ya Serikali kujiiondoa katika Mikataba hiyo imezingatiwa.

Naomba kutumia nafasi hii kuelezea japo kwa ufupi na kwa ujumla manufaa ya uwekezaji huu kwa Serikali na TPA kama ifuatavyo;

Mtazamo wa TPA kwa DP World

Inatoka Uk. 18

Ongezeko la ufanisi kwa huduma zitakazotolewa kwa meli na shehena hali itakayovutia meli nyingi zaidi na shehena kubwa ya mzigo itakayohudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam.

Pia uboreshaji wa huduma za bandari kwa kupunguza muda wa kuchakata nyaraka kwa kutumia mifumo ya kisasa ya Tehama ya Bandari itakayofungamanishwa na wadau wote wa Bandari.

Kuongezeka kwa mapato ya Serikali hususan ya ushuru wa forodha kufuatia ongezeko la shehena na meli pamoja na udhibiti wa udanganyifu kupitia mifumo ya kisasa ya bandari ikakayofungamanishwa na mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Kuongezea uzoefu TPA na kuwajengea uwezo wafanyakazi na watazania katika uendeshaji wa Bandari kwa viwango vya kimataifa.

Kuimarisha nafasi wa ushindani wa Bandari ya Dar es Salaam kikanda na kimataifa; ajira kwa watumishi wa TPA na ajira mpya kwa watazania kufuatia kupanuka kwa wigo wa shughuli za uendeshaji wa Bandari.

Kupungua kwa gharama za kusafirisha mizigo kupitia bandari ya Dar es Salaam.

Kuwepo kwa meli za moja kwa moja kutoka bara la Mashariki ya Kati kuja Tanzania ikilinganishwa na hivi sasa ambapo mizigo ya Tanzania huja kupitia nchi jirani.

Siku za kusafirisha mizigo kutoka Mashariki ya Kati na Mbali zitapungua kutoka siku 30 za sasa hadi siku zisizozidi 15.

Kuchochea ukuaji wa Sekta nyingine za Uchukuzi kama vile reli na barabara kufuatia ongezeko la shehena linalotakiwa kusafirishwa kutoka bandarini kwenda sehemu nyingine, na kuchagiza na

kuchochea shughuli nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji, usafirishaji wa madini pamoja na biashara.

Hivyo basi, naomba kutoa rai kwa watazania kujipanga na kuhakikisha kuwa wanatumia vyema fursa mbalimbali zitakazojitokeza kufuatia uwekezaji huu ikiwemo usafirishaji wa mizigo kutoka bandarini, vifungashio na vifaa mbalimbali vya kufunga mizigo pamoja na huduma mbalimbali za kuongeza thamani ambazo katika Mikataba ya uwekezaji, Serikali imehakikisha fursa hizi wanapewa wazawa (Watazania).

Uwekezaji huu wa kihistoria ni mwanzo wa safari ndefu ya uwekezaji wa kimkakati ambao Serikali inategemea kuufanya kama vile uwekezaji katika Kanda Huru za Kiuchumi (Free Economic Zone) katika Bandari Kavu ya Kwala ambapo huduma mbalimbali ikiwemo zile na kuongeza thamani bidhaa za ndani na nje ya nchi na baadae kuzisafirisha kupitia Bandari zetu au njia nyingine yoyote ya usafirishaji.

Uwekezaji wa kimkakati unaoendelea kufanywa na TPA, unatarajiwa kutoa suluhisho la changamoto za muda mrefu kwa wakulima, wafugaji na wazalishaji mbalimbali kwa kuwafungulia fursa za uhakika za masoko za kimataifa.

Menejimenti ya TPA inapenda kutoa shukrani pekee kwako na na Serikali yako ya Awamu ya Sita kwa kuelekeza, kusimamia na kuratibu vyema mapinduzi haya ya Sekta ya Uchukuzi.

Tunapenda kukuhakikishia kwamba, TPA ipo tayari kusimamia kikamilifu na kwa uzalendo mkubwa utekezaji wa Mikataba hii ili kuhakikisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wananchi wote wanaendelea kunufaika na matokeo ya uwekezaji huu wa Bandari ya Dar es Salaam.

NIKUNONG'ONEZE KWANZA



Mkuu wa Polisi wa Mkoa wa Songwe, Theopista Malya akimsikiliza mwanafunzi wa Shule ya Msingi Ichenjezya, iliyo Mbozi mara baada ya kumaliza kuwaelewa wanafunzi wa shule hiyo kuhusu utekelezaji wa program ya kuelimisha watoto juu ya kuepuka mitego inayowekwa na watu wenye nia ovu wakiwemo wabakaji. (Picha kutoka kurasa za mitandao kijamii ya Jeshi la Polisi Tanzania)

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.